# Kuanzishwa Kwa Baraza La Ushindani

Baraza la Ushindani au kwa lugha ya kiingereza "The Fair Competition Tribunal - FCT", ni chombo cha Rufaa kilichoanzishwa ***chini ya Kifungu cha 83 (1) cha Sheria ya Ushindani Na. 8 ya mwaka 2003 (The Fair Competition Act, No. 8 of 2003).*** Sheria hii inalenga kukuza na kulinda ushindani wa kibiashara na kumlinda mlaji dhidi ya matokeo ya ukiritimba na tabia potofu katika soko kwenye uchumi wa soko.

# Muundo Na Uongozi Wa Baraza

Baraza la Ushindani linaundwa na Mwenyekiti na wajumbe sita ***kwa mujibu wa kifungu cha 83(2) cha Sheria ya Ushindani ya mwaka ,2003.*** Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wote huteuliwa na Mh. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na hushikilia wadhifa huo kwa kipindi cha miaka mitatu. Mwenyekiti ni Jaji wa Mahakama Kuu. Wajumbe ni watu wenye utaalamu na uzoefu katika masuala ya kisekta, hususan uchumi, sheria, biashara, viwanda na utawala. Mwenyekiti pamoja na Wajumbe hufanya kazi pale wanapohitajika yaani "on part time basis".

Aidha, Baraza lina menejimenti ambayo ndio inahusika na masuala ya kila siku ya uendeshaji wake. Menejimenti hii inaongozwa na Msajili ambaye ni Mwanasheria anayeteuliwa na Waziri mwenye dhamana baada ya kushauriana na Jaji Mkuu chini ya ***Kifungu cha 86 cha Sheria ya Ushindani Na 8 ya mwaka 2003.*** Wengine ni Mshauri wa Sheria, Mshauri wa Uchumi na Meneja wa Fedha na Utawala. Vilevile wapo maafisa wataalamu pamoja na watumishi wa kada mbalimbali za utawala.

# Mamlaka ya Baraza la Ushindani

Mamlaka ya Baraza yameainishwa kwenye Sheria ya Ushindani Na. 8 ya mwaka 2003, Kanuni za Baraza za mwaka 2012, na Sheria mbalimbali zinazounda Mamlaka za Udhibiti. Chini ya Sheria hizo Baraza la Ushindani lina Mamlaka ya kupokea, kusikiliza na kuamua rufaa zinazotokana na maamuzi ya Tume ya Ushindani pamoja na Mamlaka za Udhibiti zifuatazo:

- Mamlaka ya Udhibiti wa Sekta ya Maji na Nishati (EWURA);
- Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri na Usalama wa Anga (TCAA);
- Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA);
- Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Mawasiliano na Utangazaji (TCRA); na
- Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA).

Baraza liliaza kupokea, kusikiliza na kuamua kesi, kuanzia Mwezi Februari, 2007 kufuatia kuanza rasmi utekelezaji wa majukumu yake mwaka 2005.

Katika kutekeleza mamlaka yake, kwa mujibu wa Kanuni ya ***38 ya Kanuni za Baraza la Ushindani za 2012,*** Baraza linaweza kufanya, kwenye shauri la rufaa, lolote kati ya haya yafuatayo:-

1. Kuthibitisha, kugeuza au kubadilisha uamuzi wa Tume ya Ushindani au Mamlaka ya Udhibiti husika.
2. Kurejesha shauri kwenye Tume ya Ushindani au Mamlaka ya Udhibiti husika pamoja na maelekezo litakayoona yanafaa kutolewa.
3. Kuamuru Tume ya Ushindani au Mamlaka ya Udhibiti husika kuendesha shauri upya.
4. Kutoa amri yoyote muhimu kufuatia uamuzi wake kama vile:
    - kuamuru kulipwa fidia kutokana na hasara;
    - kutoa Amri ya Kizuizi/Katazo;
    - kutoa adhabu kama vile faini;
    - kutoa Amri-Tamko; na
    - kuamuru kulipwa gharama za kesi.
5. Kukaza Hukumu na Amri zake.